TANGAZO LA SERIKALI Na……………….…. la tarehe………..………

**KANUNI**

SHERIA YA UTOAJI WA LESENI ZA USAFIRISHAJI,
(SURA YA. 317)

(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 45)

# KANUNI ZA LESENI MAALUM ZA SHERIA YA UTOAJI WA LESENI ZA USAFIRISHAJI, 2024

## MPANGILIO WA KANUNI


SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

*Kanuni* *Jina*

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
MAOMBI NA UTOAJI WA LESENI MAALUM

4. Sifa za leseni maalum.
5. Maombi ya leseni.
6. Uchapishaji wa notisi.
7. Uchunguzi.
8. Kutoa leseni.
9. Kukataa kutoa leseni.

SEHEMU YA TATU
MASHARTI YA LESENI MAALUM

10. Masharti ya leseni maalum.
11. Taarifa ya kubadilisha shughuli.
12. Kuhuisha leseni.
13. Ada na tozo nyinginezo.
14. Ufuatiliaji wa mara kwa mara.

SEHEMU YA NNE
USITISHAJI NA UFUTAJI WA LESENI

15. Usitishaji na ufutaji wa leseni.
16. Notisi ya utetezi.
17. Notisi ya kufanya marekebisho.
18. Kurejeshewa leseni.
19. Ukomo wa huduma.
20. Hatua za Mpito.
21. Mapitio.

SEHEMU YA SABA

MASHARTI YA JUMLA

22. Makosa na adhabu.
23. Taarifa ya usitishaji.
24. Mabadiliko.

MAJEDWALI

SHERIA YA UTOAJI WA LESENI ZA USAFIRISHAJI
(SURA YA. 317)

---

KANUNI

---

(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 45)

---

# KANUNI ZA LESENI MAALUM ZA SHERIA YA UTOAJI WA LESENI ZA USAFIRISHAJI, 2024

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

**1.** Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Leseni Maalum za Sheria ya Utoaji wa Leseni za Usafirishaji za mwaka 2024.

Matumizi

**2.** Kanuni hizi zitatumika kwa ajili ya magari ya abiria yanayofanya kazi chini ya leseni maalum kwa Tanzania Bara.

Tafsiri

**3.** In these Regulations, unless the context otherwise requires-

Sura ya. 317

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Utoaji Leseni za Usafirishaji;

Sura ya. 413

"Mamlaka" itakuwa na maana kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini;

"leseni maalum" maana yake ni leseni iliyotolewa kwa mmiliki wa leseni na Mamlaka, kwa kushauriana na Waziri, kutoa huduma maalum za usafiri wa umma katika maeneo ya mjini au sehemu yake kupitia njia au kati ya maeneo hayo kwa muda maalum;

"mmiliki wa leseni" maana yake ni shirika au kampuni iliyopewa leseni maalum ya kutoa huduma maalum za usafiri wa umma;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na masuala ya uchukuzi;

"safu ya kutosha" maana yake ni jumla ya idadi ya magari yenye muundo au uwezo tofauti wa kukapika abiria yakisafiri katika njia au eneo maalum ili kukidhi mahitaji ya abiria;

## SEHEMU YA PILI
## MAOMBI NA UTOAJI WA LESENI MAALUM

Sifa za leseni maalum

4.-(1) Ushirika au kampuni itakuwa na sifa ya kupewa leseni maalum pale ambapo-

Sura ya. 212 na Sura ya. 311

(a) limesajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni au limeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika au hati yoyote ya kisheria;

(b) lina mkurugenzi au mtu wa menejimenti ambaye hajawahi kutiwa hatiani na kosa lolote;

(i) dhidi ya usalama wa nchi;

(ii) dhidi ya uchumi wa nchi;

(iii) udanganyifu, kughushi, rushwa au makosa ya uhujumu uchumi;

(iv) kutolipa au kukwepa kodi yoyote au ushuru unaolipwa chini ya sheria yoyote ; na

(v) dhidi ya adabu au maadili

(c) halijatangazwa kuwa limefilisika;

(d) hana historia ya ukiukwaji wa kanuni za ulinzi na usalama za ndani na za kimataifa; na
(e) lina safu ya kutosha ya magari.

(2) Mkurugenzi au mtu wa menejimenti atajaza kiapo akithibitisha kuwa hajawahi kutiwa hatiani kwa makosa yaliyoainishwa kwenye kanuni ndogo ya (1)(b).

Sura ya. 212 na Sura ya. 311

(3) Kwa madhumuni ya kanuni hii, neno neno "mkurugenzi" linamaanisha mkurugenzi wa kampuni iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni na "mwanachama wa menejimenti" maana yake ni mwanachama mwandamizi wa chama cha ushirika kilichosajiliwa chini ya Sheria ya Vyama vya Ushirika au chombo kingine chochote cha kisheria.

Maombi ya leseni

5.-(1) Ushirika au kampuni inayotarajia kutoa huduma maalum za usafirishaji litaomba leseni kwa Mamlaka kwa njia ya kielektroniki.

(2) Maombi ya leseni yatakayofanywa chini ya kanuni ndogo ya (1) yataambatishwa na vifuatavyo:
(a) katiba ya kampuni au hati nyingine ya kisheria iliyoanzisha kampuni au shirika;
(b) cheti cha usajili;
(c) ripoti itakayojumuisha maelezo ya wigo wa huduma zinazotarajiwa kutolewa;
(d) mpango wa biashara;
(e) mpango wa usalama;
(f) mpango wa kukabiliana na dharura;
(g) taarifa ya hesabu ya fedha iliyokaguliwa karibuni;
(h) utaratibu wa kushughulikia malalamiko;
(i) nyaraka nyingine zozote ambazo Mamlaka itahitaji;
(j) taarifa ya benki ili kuthibitisha uwezo wa kifedha;
(k) mpango wa kuwashirikisha au kuwalipa fidia watoa huduma waliopo wanaotumia njia ambazo leseni maalum inaombwa;
(l) nauli inayopendekezwa;
(m) muundo wa taasisi unaojimuisha idadi ya wafanyakazi, uzoefu wa huduma za barabara na mchanganuo wa vitengo vya taasisi;
(n) mpango na ratiba ya matengenezo;
(o) wajibu na makatazo kwa abiria;
(p) utaratibu wa kuwahudumia walemavu na wasiojiweza kwenye treni;
(q) nakala iliyothibitishwa ya kibali kutoka kwa meneje wa miundombinu; na
(r) uthibitisho wa malipo ya ada za maombi ya leseni

(3) Maombi ya leseni maalum yatawasilishwa katika Fomu iliyoainishwa chini ya Jedwali la Kwanza.

Uchapishaji wa notisi

6. Mara baada ya kupokea maombi ya leseni maalum, Mamlaka, itatoa notisi kwenye Gazeti la Serikali a nia yake ya kutoa leseni hiyo, na leseni hiyo haitatolewa hadi kipindi cha miezi mitatu baada ya tarehe ya kuchapishwa kwa notisi hiyo.

Uchunguzi

7. Baada ya muda wa notisi kuisha kama ilivyoainishwa chini ya kanuni ya (7) Mamlaka itafanya uchunguzi.

Kutoa leseni

8. (1) Mamlaka, kwa idhini ya Waziri na kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa, itatoa leseni maalum kwa mwombaji aliyekidhi vigezo.

(2) Pale ambapo Mamlaka itatoa leseni maalum chini ya Kanuni hizi itachapisha notisi ya utoaji kwenye Gazeti la Serikali..

(3) Mmiliki wa leseni ataanza kufanya kazi ndani ya miezi sita baada ya kuchapishwa kwa notisi ya utoaji wa leseni maalum.

(4) Endapo mmiliki wa leseni atashindwa kuanza kazi bila sababu za msingi ndani ya muda ulioainishwa katika kanuni ndogo ya (3) leseni hiyo itasitishwa.

Kukataa kutoa leseni

9. (1) Mamlaka inaweza, baada ya kufanya tathmini kukataa kutoa leseni maalum na itamjulisha mwombaji kwa maandishi sababu za kukataliwa.

(2) Mwombaji ambaye maombi yake yamekataliwa anaweza kurekebisha mapungufu yaliyobainika na kuwasilisha upya maombi ndani ya siku thelathini tangu tarehe ya kupokea taarifa ya kukataliwa..

(3) Mwombaji atakayeshindwa kuwasilisha tena maombi ndani ya muda uliowekwa chini ya kanuni ndogo ya (2), atalazimika kuwasilisha maombi mapya

## SEHEMU YA TATU
## MASHARTI YA LESENI MAALUM

Masharti ya leseni maalum

10.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi, mmiliki wa leseni maalum atatimiza masharti yafuatayo-

(a) atahakikisha kuwa, hafanyi mabadiliko ya shughuli za leseni bila ridhaa ya maandishi kutoka kwa Mamlaka;
(b) wanachama wake wawili au zaidi katika kampuni iliyosajiliwa au shirika wana uzoefu katika usimamizi wa usafiri wa umma wa barabarani au kuajiri mtu aliye na ujuzi na uzoefu wa angalau miaka mitano katika usimamizi wa usafiri wa barabara;
(c) awe na safu bora ya magari kama Mamlaka itakavyoamua;
(d) awe anamiliki idadi ndogo ya magari ya usafiri wa umma kama itakavyoamuliwa na Mamlaka;
(e) awe anamiliki magari ambayo yanakidhi viwango na vigezo vilivyowekwa na mamlaka husika;
(f) awasilishe kwa Mamlaka taarifa ya hesabu ya fedha iliyokaguliwa ndani ya miezi mitatu baada ya kila mwaka wa fedha kuisha;
(g) awashirikishe au kuwalipa fidia watoa huduma waliopo wanaotumia njia ambazo leseni maalum imetolewa;
(h) afanye kazi zake ndani ya maeneo ya mjini au katika njia kati ya maeneo hayo;
(i) atahakikisha mifumo yake ya uendeshaji inaunganishwa na mifumo ya Mamlaka;
(j) atatengeneza mfumo wa kielektroniki wa kutoza nauli wenye uwezo wa kutoa mrejesho kwa abiria, kwa kulinganisha nauli inayolipwa na umbali uliosafiri;
(k) ataajiri madereva na wafanyakazi waliothibitishwa na kusajiliwa na Mamlaka; na
(l) mmiliki wa leseni wakati wote atadumisha mwenendo mzuri, uwezo wa kitaaluma na uwezo wa kifedha.

(2) Mmiliki wa leseni atafanya malipo ya ada na tozo za Mamlaka kwa wakati.

Taarifa ya kubadilisha shughuli

11.-(1). Mmiliki wa leseni ataitaarifu Mamlaka na kuwasilisha leseni kwa ajili ya mapitio pale ambapo-

(a) kuna mabadiliko katika mawanda na namna ya uendeshaji; na
(b) kuna mabadiliko katika umiliki wa hisa; au

(2) Leseni iliyotolewa chini ya Kanuni hizi haitahamishwa umiliki bila idhini ya Mamlaka

Kuhuisha leseni

12.-(1) Mmiliki wa leseni anayetaka kuhuisha leseni ataomba kwa Mamlaka ndani ya siku thelathini kabla ya tarehe ya kuisha kwa muda wa leseni.

(2) Mamlaka inaweza kutoza asilimia hamsini zaidi ya ada ya leseni kwa maombi yaliyowasilishwa siku kumi na nne baada ya kumalizika muda wa leseni na riba ya asilimia tano ya kiasi kilicholimbikizwa kila baada ya siku thelathini kwa muda usiozidi miezi kumi na mbili.

(3) Mamlaka haitazingatia maombi ya kuhuisha leseni kwa mtoa huduma ambaye ana malimbikizo ya adhabu kwa maombi yaliyowasilishwa.

Ada na tozo nyinginezo

13.-(1) Mwombaji atalipa kwa Mamlaka ada na tozo nyinginezo kwa ajili ya leseni kwa kiwango kilichoainishwa chini ya Jedwali la Pili.

(2) Ada na tozo nyinginezo zinazolipwa chini ya Kanuni ndogo ya (1) zitalipwa kwa Mamlaka na kuthibitishwa kwa risiti.

Ufuatiliaji wa mara kwa mara

14.-(1) Ili kuhakikisha uzingatiaji wa masharti ya leseni, Mamlaka itafanya ufuatiliaji wa mara kwa mara kwenye majengo na miundombinu ya mtoa huduma.

(2) Mamlaka inaweza, wakati wa kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara-

(a) kuingia, kukagua na kuhakiki kumbukumbu zozote za utendaji wa mwendeshaji;
(b) kufanya mahojiano na kuchukua maelezo ya maandishi kutoka kwa mfanyakazi yeyote;
(c) kuhakiki na kufanya uchunguzi kuhusu hali ya safu ya magari; na
(d) kutoa notisi ya maandishi inayoelekezwa kwa mwendeshaji kumtaka ajibu au kutoa taarifa ya hoja zilizoibuliwa na Mamlaka.

## SEHEMU YA NNE
## USITISHAJI NA UFUTAJI WA LESENI

Usitishaji na ufutaji wa leseni

15.-(1) Mamlaka inaweza kusitisha au kufuta leseni iwapo-

(a) mtoa huduma atashindwa kutoa huduma iliyokusudiwa ndani ya miezi sita tangu tarehe ya kuanza kutumika kwa leseni
(b) mtoa huduma ametoa taarifa ya udanganyifu kwenye maombi ya leseni; na
(c) mmiliki wa leseni ameshindwa kutii masharti yoyote ya Kanuni hizi.

Isipokuwa kwamba, kufutwa au kusitishwa hakutafanyika bila ya idhini ya Waziri.

(2) Mamlaka inaweza kumuamuru mwenye leseni kurekebisha kasoro za kiutendaji, mapungufu au masharti yoyote ambayo kwa maoni yake yamekiukwa kuhusiana na leseni.

Notisi ya utetezi

16.-(1) Endapo mmiliki wa leseni atashindwa kufuata masharti ya Kanuni hizi, Mamlaka inaweza kutoa notisi ya kumtaka mmiliki huyo kuwasilisha utetezi juu ya sababu za kutositishwa au kutofutwa kwa leseni ndani ya siku ishirini na moja tangu tarehe ya notisi.

(2) Endapo mtoa huduma atashindwa kujibu ndani ya muda ulioainishwa katika Kanuni ndogo ya (1) au Mamlaka haijaridhishwa na sababu zilizotolewa na mtoa huduma, Mamlaka inaweza, kwa kuzingatia idhini ya Waziri, kusitisha au kufuta leseni ndani ya siku ishirini na nane.

(3) Mamlaka inaweza pale inapoona inafaa, kufanya uchunguzi kabla ya kutekeleza jukumu la kusitisha au kufuta leseni maalum.

Notisi ya kufanya marekebisho

17.-(1) Endapo Mamlaka itabaini mapungufu yanayosababisha mtoa huduma kutokidhi vigezo vya Sheria au Kanuni hizi, Mamlaka inaweza kutoa notisi ya kufanya marekebisho ili kurekebisha mapungufu ndani ya muda ulioainishwa kwenye notisi.

(2) Notisi ya kufanya marekebisho inayotolewa chini ya Kanuni ndogo ya (1) itakuwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Nne.

Kurejeshewa leseni

18. Ikitokea leseni imesitishwa, Mamlaka inaweza kurejesha leseni baada ya kutimiza masharti kama yalivyoainishwa kwenye notisi ya usitishwaji.

Ukomo wa huduma

19.- Endapo leseni iliyotolewa chini ya Kanuni hizi imesitishwa au imefutwa, mtoa huduma ataacha kutoa huduma.

Mpito

20. Endapo leseni imesitishwa au kufutwa chini ya Kanuni hizi, Mamlaka itachukua hatua za mpito ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya usafiri kwa njia hiyo.

Mapitio

TS Na. 73 la 2020

21. Mtu ambaye hajaridhishwa na uamuzi wa Mamlaka chini ya Kanuni hizi anaweza, ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya uamuzi huo, kutuma maombi kwa Mamlaka kwa ajili ya mapitio kwa utaratibu ulioainishwa na Kanuni za Mapitio za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini.

## SEHEMU YA SABA
## MASHARTI YA JUMLA

Makosa na adhabu

22. Mtu atakayekiuka au kushindwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi milioni tatu au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

Taarifa ya usitishaji

23. Pale ambapo mmiliki wa leseni anakusudia kusitisha shughuli zake, ataitaarifu Mamlaka, kwa maandishi, miezi sita kabla ya kusitishwa huko.

Mabadiliko

24. Pale ambapo mmiliki wa leseni anakusudia kuongeza au kupunguza idadi ya magari ataomba kwa Mamlaka mabadiliko kwa kulipa ada kama zilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5 (3))*

## FOMU YA MAOMBI YA LESENI MAALUM

Jina la Kampuni: ………………………………………………………..………….

Namba ya Usajili. ……………………..……………………………..

Tarehe Iliyotolewa: ……………………………………………………………..………….

Eneo la Biashara Lililosajiliwa: ……………………………………..……………........

Anuani ya Makazi: ……………………………….……………………………………

S.L.P: …………………………………………………………………………

Namb ya Simu: ………………………………………………………..……………...

Barua Pepe: …………………………………………………………………………

**Jedwali la Taarifa za Umiliki wa Hisa:**

| Jina | Uraia | Anuani | Asilimia |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |

**AINA YA LESENI INAYOOMBWA**

| SN | Aina ya Huduma Inayotolewa | Chagua Inayofaa |
|---|---|---|
| 1 | Huduma za Abiria | |
| 2 | Huduma za Abiria Mijini | |
| 3 | Huduma za Mizigo | |

**Maelezo mafupi na mawanda ya huduma itakayotolewa**:

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

**Taarifa ya leseni iliyoisha (kama ipo) Namba**: ………………………. Tarehe ya kuisha ……………………

Taarifa ya jumla, ikiwemo kumbukumbu juu ya rasilimali fedha za Mwombaji (Ambatanisha kurasa za ziada ikiwa ni lazima).
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

Mimi …………………………………………………… natamka kwamba maelezo yaliyotolewa katika maombi haya ni ya kweli, sahihi na kamili kwa kadri ya ufahamu wangu. Ninaelewa kwamba kutoa taarifa zozote za uongo kunaweza kusababisha kukataliwa kwa ombi hili au kubatilishwa kwa leseni.

**Jina Kamili:** ……………………………………………………………………………..…

**Cheo:** ………………………………………………………………………………

**Sahihi:** ……………………………………………………………………………...…

**Muhuri:** ……………………………………………………………………………...

**Tarehe:** ………………………………………………………………………………………

## JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 14)*

**ADA**

| **UWEZO WA KUBEBA ABIRIA** | **ADA KWA MWAKA (TZS)** | | | |
|---|---|---|---|---|
| Inayozidi abiria 45 lakini haizidi abiria 65 | 400,000 | | | |
| Inayozidi watu 65 | 500,000 | | | |
| Ada za maombi za mwaka | 20,000 | | | |
| Ada ya kubadili leseni | Asilimia hamsini (50%) ya ada za mwaka | | | |
| **HUDUMA NYINGINE** | | | | |
| Cheti cha Usajili kwa Kampuni ya Usafirishaji | | | | 100,000 |

## JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 21(2))*

---

NOTISI YA MAREKEBISHO

**Kwa:** …..........................................................

Ninakupa notisi kwa mujibu wa Kanuni ya 22(2), kwamba baada ya siku ………………..kuanzia tarehe ya kupokelewa notisi hii, ninakusudia……………………………………….(eleza hatua zinazokusudiwa kuchukuliwa kupunguza hatari) isipokuwa,kabla ya kuisha kwa muda uliowekwa, utetetezi wa kuniridhisha uwe umetolewa kuonesha hatua ulizochukua kurekebisha usalama wa reli au hatua nyingine yoyote iliyochukuliwa kurekebisha mapungufu.

Maeneo yanayohitaji marekebisho ni:

1) …..........................................................................................................................
2) …..........................................................................................................................
3) …..........................................................................................................................
4) …..........................................................................................................................
5) …..........................................................................................................................

**Imetolewa** …………………...……. **tarehe**….............. **mwezi** …....................................... **20**……...
**Sahihi**.......................................................................................................................
**Jina la Mkaguzi.**.......................................................................................................

Dodoma, MAKAME MNYAA MBARAWA

........................... 2024 *Waziri wa Uchukuzi*